

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole  
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MAGANZO (MAGANZO WSSA) KWA MWAKA 2018/19

Mnamo tarehe 26 Februari 2019, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi ya marekebisho bei na ada kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maganzo. Maombi hayo yametokana na kubadilika kwa gharama za maji ya jumla kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga (KASHWASA) kwa kuongezeka kwa asilimia 38 na kuanza kutekelezwa 1 Januari 2019. Jedwali hapa chini yanaonesha muhtasari wa maombi hayo.

#### Jedwali 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi (Shilingi/Uniti)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadili ko kwa asilimia	2018/19	Mabadili ko kwa asilimia	2019/20	Mabadili ko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	1,520	(5%)	1,440	4%	1,500	3%	1,540
Taasisi	1,520	30%	1,980	4%	2,060	7%	2,200
Biashara	1,520	31%	1,995	5%	2,100	10%	2,310
Viwanda	1,520	93%	2,930	0%	2,930	2%	3,000
Kuosha magari	-	-	2,400	4%	2,500	2%	2,550
Magati	1,750	9%	1,900	0%	1,900	0%	1,900

**Jedwali 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)**

Kundi la wateja	Ada za sasa	Ada zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	6,000	67%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Taasisi	6,000	67%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Biashara	6,000	67%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Viwanda	6,000	67%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Kuosha magari	-	-	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Magati	6,000	67%	10,000	0%	10,000	0%	10,000

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, EWURA inanzisha mchakato wa kupata maoni ya wadau ili kujua uhalali wa maombi iliyoyapokea.

Nakala ya maombi na nyaraka za Maganzo zilizowasilishwa EWURA zinaweza kusomwa na mtu yeyote wakati wa saa za kazi kati ya saa 3 asubuhi na saa 10 jioni katika ofisi za EWURA. Wadau wanaombwa kuzingatia muda uliopangwa ili kufanikisha zoezi hili.

Katika mchakato huo, EWURA itakusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, wakiwamo Baraza la Wawakilishi wa Watumiaji wa huduma (CCC); Baraza la Ushauri la Serikali (GCC) pamoja na wananchi. Wadau wanaopenda kutoa maoni yao wataombwa kuwasilisha maombi yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kuyatuma kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonyeshwa hapo juu ndani ya kipindi cha wiki mbili baada ya tangazo hili. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika **OFISI ZA EWURA KANDA YA ZIWA, GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF – BARABARA YA KENYATTA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MAGANZO.**

**Imetolewa na:**  
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

**10 Aprili 2019**

